

MEDIA BRIEFS OF MoM NOVEMBA 19, 2019

JAMVI LA HAHARI

- **STAMICO hii haiwezi kufutwa-Kamati ya Bunge**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika ya Umma, imesema Shirika la Taifa (STAMICO) haliwezi kufutwa tena kutokana na mwenendo wa sasa kuridhisha. Kubadilika mtazamo huo kunatokana na mwenendo wa awali kutoridhisha katika utendaji wake hali iliyofanya baadhi ya wabunge kutaka Shirika hilo lifutwe. (Uk. 5)

MAJIRA

- **Kamati ya Bunge yasisitiza STAMICO haiwezi kufutwa**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika ya Umma imesema Shirika la Taifa (STAMICO) haliwezi kufutwa tena kutokana na mwenendo wake wa sasa kuridhisha kutokana na utendaji wake kubadili mtazamo wa awali. STAMICO awali ilionekana kufanya vibaya, hali iliyopelekea baadhi ya wabunge kutaka Shirika hilo lifutwe ambapo kwa sasa wameshuhudia mabadiliko makubwa yenye tija kwa taifa. (Uk. 2)

NIPASHE

- **Tancoal yampongeza JPM kuleta mapindizi**

KAMPUNI ya kuzalisha Makaa ya Mawe (Tancoal) imempongeza Rais John Magufuli kwa kuleta mapinduzi chanya kwenye sekta ya madini nchini katika kipindi cha miaka minne ya utawala wake. Taarifa iliyotolewa jana na kampuni hiyo ilieleza kuwa katika kipindi cha miaka minne imeongeza uzalishaaji wa Makaa ya Mawe nchini.(Uk. 26)

MWANANCHI

- **HABARI PICHA**

Wafanyabiashara jijini Arusha wakimsikiliza Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo wakati wa mkutano uliofanyika katika Soko la Madini jana kabla ya wafanyabiashara hao kuanza kufanya shughuli zao eneo hilo. (Ukurasa wa mbele)

THE CITIZEN

- **STORY PICTURE**

Mineral traders attend a meeting addressed by Minerals Deputy Minister Stanslaus Nyongo in Arusha yesterday. Mr Nyongo was

on an inspection tour of the Arusha regional minerals trading centre, which was opened in June.